TANGAZO LA SERIKALI Na. 315 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA IHEGA - BUKOLI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Ihega - Bukoli ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

*Tangazo la Serikali Na.315 (Linaendelea.)*

________

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 421699MS, 9941353KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS73°MG kwa umbali wa kilomita 2.96 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 419795MS, 9639090KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS91°MS kwa umbali wa kilomita 7.37 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 4265568MS, 9636170KZ); baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ131°MS kwa umbali wa kilomita 2.91 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 427781MS, 9638815KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Maghribi katika uelekeo wa116°kwa umbali wa kilomita 2.67 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 426684MS, 9641245KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa KZ129°MS kwa umbali wa kilomita 4.99 hadi ulipoanzia""

| | |
|---|---|
| Dodoma, | ANGELINE S. MABULA, |
| 17 Machi, 2023 | *Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi* |